JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA
MKOA WA NJOMBE
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE
SIMU: 0628043943, 0764817475, 0675886744, 0754588298, 0754977045, 0766342580

SHULE YA SEKONDARI LUPILA,
S.L.P 602,
NJOMBE – MAKETE.
03/12/2020

KUMB. NA.MK/DC/LSS/JI/129

MWANAFUNZI _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPILA KIDATO CHA KWANZA 2021

1. Nina furaha ya kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza katika Shule hii Mwaka 2021.
2. Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 siku ya Jumatatu asubuhi. Unatakiwa kuripoti bila kukosa shuleni tarehe 11/01/2021.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
MCHANGO WA CHAKULA KWA WANAFUNZI WA HOSTELI

Kwa kuwa kila Mwanafunzi atakaa Hosteli hivyo:-

Kila mzazi atamchangia mtoto wake chakula kwa utaratibu wa miezi mitatu mitatu yaani robo mhula. Gharama ya chakula kwa mwaka ni Tsh. 380,000/=. Hivyo utachangia kama ifuatavyo:-

Robo ya 1 Jan - Mach	Robo ya 2 April - Juni	Robo ya 3 Julai - Sept	Robo ya 4 Okt - Dese
95,000/=	95,000/=	95,000/=	95,000/=

Pia Mzazi atachangia mchango wa majiko na masufuria 20,000/=

Kwa gharama hiyo ni makubaliano ya Wazazi baada ya kukubaliana bajeti ya Mwaka 2020. Mwanafunzi atakula chakula kama ifuatavyo:-

- Uji kila siku
- Ugali maharage milo miwili kila siku
- Nyama mara moja kwa mwezi
- Wali mara moja kwa wiki
- Mboga za majani kila siku na matunda mara 2 kwa wiki
- Pia fedha hiyo italipa wapishi wa chakula cha wanafunzi

3. SARE YA SHULE

A: Sare ya shule ni:

i. Kwa Wavulana:- Suruali mbili (2) nyeusi na kijani jeshi kitambaa kizito zenye mshono wa heshima (suruali zenye mfuko wa jeans haziruhusiwi), shati mbili (2) tetroni mikono mirefu, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba (gidamu) vyenye kisigino kifupi jozi mbili (2), soksi nyeusi jozi tano (5) sweta la bluu lisilo na maandishi yeyote na T-shirt nyekundu (itapatikana shuleni yenye nembo ya shule), track – suit nyeusi (adidas), raba nyeusi na Neti.

ii. Kwa Wasichana:- Suruali mbili (2) nyeusi na kijani jeshi kitambaa kizito zenye mshono wa heshima, Gauni solo mikono mirefu (2) rangi nyeupe satini malinda na isiyo malinda, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba (gidamu) vyenye kisigino kifupi jozi mbili (2),

soksi nyeupe ndefu jozi tano (5) sweta la bluu lisilo na maandishi yeyote na T-shirt nyekundu (itapatikana shuleni yenye nembo ya shule), track – suit nyeusi (adidas), raba nyeusi na Neti.

B: SARE ZA MICHEZO NA NGUO ZA KUSHINDIA/KAZI ZA NJE.

i. **Kwa Wavulana:-** Raba nyeusi na nyeupe jozi moja, Bukta bluu au nyeusi na fulana (T-shirt nyekundu na track suit nyeusi (adidas) na surual Dark bluu. Pia aje na chelewa kubwa (mfagio) na mfagio mgumu wa kudekia 1 (Hard Broom)

ii. **Kwa Wasichana:-** Raba nyeusi, gauni rangi ya pink (solo) na truck suit nyeusi (adidas)
NB: Sare zote zilizotajwa na kuainishwa hapa juu mwanafunzi anunue na kuja nazo siku ya kuripoti shuleni na ziwe katika maadili ya shule na ukishona tofauti hutapokelewa (sare za kushona kama suruali, Blauzi, magauni atapimwa shule, Mzazi atapatana na fundi hapa shuleni).
- Kitanda shilingi 60,000/=

4. VIFAA VYA DARASANI NA VINGINEVYO

a) Mkebe wa hisabati (Mathematical sets) Daftari kubwa 15 (counters) na kalamu(bick) za kutosha, Kamusi ya kisswahili na kingereza, Biblia kwa wakristo na kuluani kwa waislamu. Pia aje na bunda la karatasi kwa ajili ya matumizi yake ya mazoezi ya kila wiki (Ream)1.

5. VIFAA VYA HOSTELI

a) Ndoo mbili kwa ajili ya kuogea na usafi
b) Godoro la futi 2½ (upana), Blanketi moja na shuka mbili (2) rangi ya pinki.
c) Vyombo vya kulia chakula (sahani, bakuli , kikombe na kijiko)
d) Kitanda uje na fedha shilingi 60,000/=
e) Neti
f) Uje na fedha ya umeme shilingi 10,000/= kwa mwaka
g) Mfagio mkubwa 1(chelewa), mfagio wa kudekia 1 (rubber squeezer) na brashi ngumu 1 (Hard broom).

6. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayuo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapata nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi na wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi na kutimiza shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hivyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

Muhimu: Kila Mwanafunzi aje na picha 3 za paspoti kwa matumizi ya Ofisi. Aidha huduma hii itapatikana hapa shuleni.

7. Makosa yafuatayo yanaweza yakasababisha ukafukuzwa shule
(a) Wizi

(b) Uasherati, ubakaji na ushoga
(c) Ulevi na madawa ya kulevya
(d) Uvutaji bangi
(e) Makosa ya jinai
(f) Kupigana na kupiga
(g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(h) Kudharau bendera ya shule
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kupata mimba au kusababish amimba ndani ya shule
(k) Kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba
(l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi.

8. MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA

(a) Wasichana wote na wavulana wote lazima kukaa Hosteli
(b) Kwa wanafunzi wote ni vema kuleta fedha kama ilivyoainishwa hapo juu
(c) Jaza fomu ya kupima afya yako (Medical examination form) kwa mganga wa Wilaya au kituo cha afya
(d) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu Historia ya wanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
(e) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa, michango na maelezo mengine yatatolewa shuleni
(f) Mahitaji muhimu yaliyoainishwa hapo juu ikiwa ni pamoja na, michango ya chakula, sare, vifaa na fomu mbalimbali vyote vitakaguliwa siku anaporipoti mwanafunzi shuleni. Visipo kamilika utarudishwa kuvifuata.
(g) Mwisho wa kumpokea mtoto ni tarehe 11/01/2021 atakayechelewa atachukuliwa hatua za kisheria.

NB: FEDHA ZA CHAKULA ZINAKUSANYWA NA KAMATI MAALUMU YA WAZAZI YA CHAKULA NA KUPANGA MATUMIZI YAKE KAMA WALIVYOKUBALIANA NA MZABUNI NA WAZAZI

NB: Sare ya shule ya kushona itapatikana hapa shuleni

TAREHE YA KURIPOTI NI MOJA TU KWA WANAFUNZI WOTE HIVYO FIKA BILA KUKOSA ILI KUEPUKA UONGOZI WA KATA KUKUCHUKULIA HATUA.

9. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYO NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI LUPILA

_____

ABKASA JOHN NGWALE
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI LUPILA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE PRESIDENT'S OFFICE – RALG

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECKNOLOGY AND VOCATION TRAINING

LUPILA SECONDARY SCHOOL

M.E. FORM

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

This form must be completed by the Government medical officer.

Name of Student ……..

Age ……..sex …….

The above named student has been examined in respect of;

- PREGNANCY TEST (FOR GIRLS ONLY) ……
- STOOL ……
- URINE ……..
- CHEST ……
- BLOOD ……
- EYES ……
- EARS ……
- ASTHMA ……..
- SKIN DISEASE ……...
- LEPROSY ……
- EPILEPSY ……
- NEUROSIS ……..
- VENERAL DISEASES ……
- ANY DEFORMITY ……...
- OTHER FINDINGS ……

I am satisfied that the above named students is fit/not fit for pursuing Secondary studies at **LUPILA SECONDARY SCHOOL**.

…….. **……..**

SIGNATURE **DATE**

…… **……**

DESINATION AND OFFICIAL STAMP **STATION**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

SHULE YA SEKONDARI LUPILA

S.L.P 602,

NJOMBE.

03/12/2020

FOMU YA KUKUBALI KUPOKEA NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. Mimi Mzazi/Mlezi wa _____ninakubali kupokea nafasi ya Mtoto wangu kujiunga na Kidato cha Kwanza Lupila Sekondari na nipo tayari kutimiza mahitaji yote ya shule kwa ajili ya Mwanangu.
   Jina la Mzazi/Mlezi _____kazi _____Sahihi _____
2. Mimi _____ ndiye niliyechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Lupila. Ninakubali kupokea nafasi hii.
3. Mimi _____ Mtendaji wa Kijiji cha _____ nimethibitisha kuwa Mzazi wa mtoto amekubali kupokea nafasi hiyo na kuahidi kutoa huduma zote mpaka atakapo hitimu masomo yake
   Sahihi _____ Tarehe _____

   Mhuri wa Ofisi ya Kijiji

   NB: Fomu hii lazima ipitishwe na Mtendaji wa Kijiji

4. **Kwa matumizi ya Ofisi**
   Tarehe ya kuripoti _____
   Mkondo aliopangiwa _____
   Maoni ya Mwalimu Mlezi _____
   Sahihi _____ Tarehe _____

_____

ABKASA JOHN NGWALE
MKUU WA SHULE